**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**
**(EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO. GA.71/135/CZ/2024/09**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2024-00000185**

**KATI YA**

**PETER J. SHUGHURU ............................................................ MLALAMIKAJI**

**NA**

**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA ............................................. MLALAMIKIWA**

---

**AMRI**

---

***(Imetolewa na Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA la tarehe 23 mwezi Desemba 2025)***

**MALALAMIKO HAYA** yameletwa mbele ya Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwa ajili ya kutoa uamuzi leo tarehe 23 mwezi Desemba 2024, kwa madai kwamba Mlalamikiwa aamriwe kumrudishia Mlalamikaji uniti zake 1700 zilizokuwepo kwenye dira yake ya LUKU namba 54183420188 iliyobadilishwa baada ya kupata hitilafu ya kuungua na kuwekewa dira mpya namba 24314513144 pindi Mlalamikiwa alipokuwa anatekeleza zoezi lake la kufunga machine umba (*Transfomer)* mpya katika eneo la Mlalamikaji mnamo tarehe 17 Mei 2023.

Mlalamikiwa anapinga kwa kusema kwamba ushahidi wa uniti za umeme zinazodaiwa kuungua kwenye dira ya awali unakosekana kwa upande wa Mlalamikiwa. Na kwa ushahidi wa manunuzi kwa upande wa Mlalamikiwa,

hauwasaidii kuweza kurudisha uniti hizo za umeme zinazodaiwa, isipokuwa ushahidi wa picha ya mita inayodaiwa kuungua kuonesha uniti hizo zilizokuwepo kabla ya tatizo kutokea.

Hivyo basi Mlalamikiwa anaiomba Mamlaka itupilie mbali malalamiko haya na Mlalamikaji aendelee kufurahia huduma za Mlalamikiwa.

Taarifa ya malalamiko ilipokelewa na Mamlaka tarehe 11 Julai 2024, na waraka wa kuwasilisha utetezi ulitumwa kwa Mlalamikiwa ambapo majibu ya utetezi yalipokelewa tarehe 13 Agosti 2024. Kikao cha kwanza cha usuluhishi kilichohusisha pande zote mbili kilifanyika tarehe 19 Septemba 2024 katika Ukumbi wa ofisi za EWURA Kanda ya Kati, Ghorofa ya kwanza uliopo Dodoma Mjini na kikao cha pili pia kilifanyika mnamo tarehe 26 Novemba 2024. Katika kikao hicho, Mlalamikaji alieleza kuwa Mlalamikiwa ameshatatua tatizo lake na amemrudishia uniti 1700 alizokuwa anazilalamikia hivyo hana haja ya kuendelea na shauri hilo na kuandika barua pepe ya kuomba kuyaondoa malalamiko haya.

Katibu wa Bodi **ANATOA AMRI** kwamba malalamiko haya yameondolewa na kila upande utabeba gharama za uendeshaji wa malalamiko haya.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 23 mwezi Desemba 2024.

..............................

**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**